SHIRIKA LA RELI TANZANIA

Jarida la

RELI NA MATUKIO

Toleo namba 20, Mei 2022

Habari | Makala | Matukio | Elimu | Picha

# MHE. PROF. MBARAWA AWEKA JIWE LA MSINGI MRADI WA SGR MAKUTUPORA - TABORA




Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Mhe. Prof. Makame Mbarawa akiweka jiwe la msingi la mradi wa Ujenzi wa Reli ya Kisasa - SGR Makutupora - Tabora Aprili, 2022.

Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Mhe. Prof. Makame Mbarawa aweka jiwe la msingi la mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa – SGR kipande cha tatu Makutupora - Tabora Aprili, 2022.

Hafla hiyo imefanyika katika uwanja uliopo Cheyo "B" mkoani Tabora ikihudhuriwa na viongozi mbalimbali wa Serikali na taasisi binafsi wakiwemo mawaziri mbalimbali, katibu mkuu wa Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Balozi wa Uturuki nchini, Mkuu wa mkoa wa Tabora, wakuu wa wilaya, Kamati ya Bunge ya Bajeti, kamati ya Bunge ya Miundombinu, Mwenyekiti na Wajumbe wa Bodi ya Bodi ya Wakurugenzi Shirika la Reli Tanzania – TRC, viongozi wa chama na serikali, viongozi wa dini pamoja na taasisi binafsi.

Taasisi nyingine zilizohudhuria hafla hiyo ni Mamlaka ya Usafiri wa Ardhini (LATRA), TCB, Kampuni ya Mafuta GBP, CRDB, Kampuni ya Tigo, NMB, BRAVO Logistics, NBC, Kampuni ya PUMA, Shirika la Posta, Kampuni ya AKO, Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), Kampuni ya BAKHRESA, Kampuni ya KAMAL, SMH Rail na Shirika la Bima.

Inaendelea Uk. 2

## TRC YAANZA MAJARIBIO YA MIFUMO YA UMEME KATIKA RELI YA KISASA Uk. 4



*Wahandisi umeme kutoka Shirika la Reli Tanzania na Kampuni ya Yapi Merkezi wakiwa katika zoezi la majaribio ya mifumo ya umeme katika ofisi iliyopo kituo cha kupoza umeme Pugu jijini Dar es Salaam Aprili 27, 2022.*

# MHE. PROF. MBARAWA AWEKA JIWE LA MSINGI MRADI WA SGR MAKUTUPORA - TABORA

Inatoka Uk. 1

Akihutubia katika hafla hiyo Mhe. Mbarawa amesema kuwa ujenzi wa Reli ya Kisasa Makutupora – Tabora unahusisha ujenzi wa reli yenye urefu wa jumla ya kilomita 368 ambapo Kilomita 294 ni njia kuu na kilomita 74 ni njia za kupishania, ambapo thamani ya mkataba wa ujenzi ni Dola za Marekani bilioni 1.908 sawa na Shilingi trilioni 4.406, muda wa ujenzi ni miezi 46 ikijumlisha muda wa majaribio.

Mhe. Prof. Mbarawa ameipongeza Bodi ya Wakurugenzi, Menejimenti na Wafanyakazi wa Wizara na TRC na kuongeza kuwa Serikali itaendelea kutimiza wajibu wake wa kutoa fedha za utekelezaji wa miradi hii.

"Wajibu wetu ni kuhakikisha kuwa mnatekeleza majukumu yenu kwa weledi na umahiri mkubwa. Mfanye kazi kwa uzalendo, kwa pamoja kama timu moja, kujituma, kuongeza ubunifu na kuzingatia miongozo ya serikali" amesema Prof. Mbarawa

Mkuu wa mkoa wa Tabora Mhe. Batilda Buriani ameishukuru Serikali kwa kuamua kutekeleza mradi mkubwa wa kimkakati mkoani humo unaokwenda kuzalisha fursa za ajira na uchumi katika mkoa wa tabora.



Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Mhe. Prof. Makame Mbarawa (kati) akisalimiana na Naibu Waziri wa Ujenzi na Uhukuzi Mhe. Atupele Mwakibete (kushoto) alipowasili uwanja wa Cheyo "B" katika hafla ya uwekaji jiwe la msingi la mradi wa Ujenzi wa Reli ya Kisasa - SGR mkoani Tabora Aprili, 2022.



Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Mhe. Prof. Makame Mbarawa (kati) akikata utepe kuashiria uzinduzi wa mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa - SGR mkoani Tabora Aprili, 2022.

"Mhe Mgeni rasmi sisi tunatambua kuwa kuna fursa nyingi katika mradi huu, nakuahidi kwamba tutaulinda mradi huu, tutashirikiana na TRC katika kulinda miundombinu pia katika kuhakikisha maeneo yanapatikana ili mradi uendelee, na mimi sina wasiwasi na TRC kwasababu TRC wamedhihirisha kuwa wanajali eneo wanalofanyia kazi ndio maana TRC leo wametupa eneo kwaajili ya wajasiriamali" amesema Mhe. Batilda

Naye Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania Masanja Kadogosa katika taarifa yake ameeleza kuwa kipande cha SGR Makutupora – Tabora kitakuwa na vituo vya abiria na mizigo vipatavyo nane (8) ambavyo ni Manyoni, Itigi, Kazikazi, Tura, Malongwe, Goweko, Igalula na Tabora, pamoja na kituo cha uendeshaji treni cha dharura Tabora, hii ni endapo ikitokea hitilafu katika kituo kikuu (OCC) Dar es salaam treni ziweze kuongozewa kutokea tabora bila kusimamisha kazi za uendeshaji.

Miongoni mwa faida mabazo wananchi wa mkoa wa Tabora watazipata kupitia mradi wa SGR ni pamoja na ajira ambapo Kwa takwimu zilizopo,

mpaka sasa jumla ya ajira za moja kwa moja zimetolewa kwa watanzania 16,000. Pia, Ajira hizo zimechangia malipo ya mishahara yenye thamani ya Shilingi Bilioni 224, zabuni na kandarasi zenye thamani ya shilingi trilioni 1.776 zimetolewa kwa wakandarasi wadogo 1663. Faida nyingine ni kuwa serikali imekusanya kodi yenye jumla ya Shilingi bilioni 441.

# MATUKIO KATIKA PICHA; HAFLA YA UWEKAJI JIWE LA MSINGI MRADI WA SGR MAKUTUPORA - TABORA



Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Mhe. Prof. Makame Mbarawa (kati) akipata maelezo kutoka kwa Mkurugenzi Mkuu wa Benki ya TCB (kushoto) alipowasili uwanja wa Cheyo "B" katika hafla ya uwekaji jiwe la msingi mradi wa Ujenzi wa Reli ya Kisasa - SGR Makutupora - Tabora Aprili 2022.



Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Mhe. Prof. Makame Mbarawa (kati) akisalimiana na viongozi wa benki ya CRDB walioshiriki maon esho katika hafla ya uwekaji jiwe la msingi la mradi wa Ujenzi wa Reli ya Kisasa - SGR yaliyofanyika Cheyo "B" mkoani Tabora Aprili 2022.




Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Mhe. Prof. Makame Mbarawa (kushoto) akipata maelezo kutoka kwa Mwakilishi wa benki ya NMB Bwana Emmanuel Akonae alipowasili uwanja wa Cheyo "B" katika hafla ya uwekaji jiwe la msingi la mradi wa Ujenzi wa Reli ya Kisasa - SGR Makutupora - Tabora Aprili 2022.



Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Mhe. Prof. Makame Mbarawa (kati) akipata maelezo kutoka kwa Mwakilishi wa Benki ya NBC Bwana Godwin Semunyu (kati) alipowasili uwanja wa Cheyo "B" katika hafla ya uwekaji jiwe la msingi la mradi wa Ujenzi wa Reli ya Kisasa - SGR Makutupora - Tabora Aprili 2022.



Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Mhe. Prof. Makame Mbarawa (kati) akipata maelezo kutoka kwa Mwakilishi wa Kampuni ya Tigo Bwana Lugutu Lugutu (kushoto) alipowasili uwanja wa Cheyo "B" katika hafla ya uwekaji jiwe la msingi la mradi wa Ujenzi wa Reli ya Kisasa - SGR Makutupora - Tabora Aprili 2022.



Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Mhe. Prof. Makame Mbarawa (kulia) akipata maelezo kutoka kwa Mwakilishi wa Shirika la Posta Bwana Constantine Kazeze alipowasili uwanja wa Cheyo "B" katika hafla ya uwekaji jiwe la msingi la mradi wa Ujenzi wa Reli ya Kisasa - SGR Makutuora - Tabor Aprili 2022,

# TRC YAANZA MAJARIBIO YA MIFUMO YA UMEME KATIKA RELI YA KISASA

Shirika la Reli Tanzania – TRC kwa kushirikiana na Mkandarasi wa ujenzi wa Reli ya Kisasa – SGR kampuni ya Yapi Merkezi limeanza zoezi la majaribio ya mifumo ya umeme katika miundombinu ya reli ya kisasa Pugu jijini Dar es Salaam Aprili 2022.



Zoezi hilo ni sehemu ya majaribio ya mifumo ya umeme kwa kipande cha Dar es Salaam – Morogoro ambacho kipo katika hatua za mwisho za ujenzi kwaajili ya kuanza shughuli za uendeshaji. Uwashaji umeme katika reli ya kisasa unafanyika kwa awamu nne katika vituo vinne vya kupozea umeme ambapo majaribio yamefanyika kwa mafanikio katika kituo cha kwanza kilichopo Pugu.

Vituo vingine ni pamoja na kituo cha Ruvu, Ngerengere na Morogoro ambavyo vitafanyiwa majaribio kwa awamu huku zoezi la kupitisha kichwa cha treni cha Mkandarasi kinachotumia umeme likifanyika kwa utaratibu huo. Lengo la majaribio yanayofanywa na mkandarasi ni kuhakikisha kuwa mifumo yote iliyopo kwenye reli ya kisasa iko sawa na tayari kwaajili ya shughuli za uendeshaji bila ya kuleta madhara kwa watumiaji.

Aidha, Shirika kwa kushirikiana na Mkandarasi linaendelea na zoezi la utoaji elimu na kuhamasisha jamii kuhusu tahadhari za kuchukua na taratibu za kufuata wakati wa majaribio ya mifumo ya umeme katika reli ya kisasa.

Maeneo ambayo tayari elimu hiyo imetolewa kwa wananchi ni pamoja na Mtaa wa Guluka kwa lala, Gongo la mboto, Buguruni Sokoni, Vingunguti, Kwa Mnyamani, Kipawa mji mpya, Majumba sita, Shule ya Sekondari Ilala, Majani ya chai, Pugu stesheni, Pugu Mnadani, Sekondari ya Ukonga, Shule ya msingi Mikongeni, kata ya Gongo la Mboto, Mwembe Madafu, Ruvu na Soga.

Katika zoezi hilo wananchi wameendelea kulishukuru Shirika la Reli Tanzania kwa kujali afya na usalama wa wananchi kwa kuwapa elimu ya ulinzi na usalama katika kipindi cha majaribio ya miundombinu ya umeme wa reli ya kisasa.

Mkazi wa Gongo la Mboto Bwana Nikaro Sabai amesema kuwa “Elimu inayotolewa ni muhimu sana na ningeliomba Shirika liendelee na elimu hii ya usalama na mara kwa mara kwasababu ujenzi wa reli ya kisasa ni kitu kipya kwa jamii kwahiyo tunahitaji elimu madhubuti ili tuweze kujenga utamaduni wa kutunza na kuzingatia usalama wa reli"

Katika kuhakikisha usalama unazingatiwa ni vyema kila mwananchi kuchukua hatua madhubuti katika kufuata sheria na miongozo inayotolewa ikiwemo namna ya kuvuka kwenye miundombinu ya reli, kutoa taarifa sehemu sahihi pindi changamoto za kiusalama zinapotokea na kujenga utamaduni wa kutunza miundombinu ya reli kwa manufaa ya Taifa.

# BEHEWA 1,430 ZA KISASA ZA MIZIGO KUNUNULIWA




Mkurugenzi Mkuu wa TRC Masanja Kadogosa (kushoto) na Bwana Tang Yun Peng, Meneja Msaidizi kutoka kampuni ya CRRC International ya China wakisaini makabrasha ya mkataba wa ununuzi wa behewa 1430 za SGR kwaajili ya kubeba mizigo katika ofisi ya makao makuu TRC jijini Dar es Salaam Februari 2022

Shirika la Reli Tanzania – TRC limesaini mkataba na kampuni ya CRRC International kutoka nchini China kwaajili ya ununuzi wa Behewa 1430 za mizigo zitakazotumika katika reli ya kisasa – SGR, hafla ya utiaji saini imefanyika katika ukumbi wa mikutano makao makuu TRC Februari 2022.

Hafla hiyo imehudhuriwa na viongozi wa Serikali na Shirika, ambapo Mgeni Rasmi katika hafla hiyo alikuwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Mhe. Prof. Makame Mbarawa, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi TRC, Mkurugenzi Mkuu TRC, Wawakilishi wa kampuni ya CRRC International, Menejimenti na Wafanyakazi wa TRC pamoja na wanabari.

Mhe. Prof. Makame Mbarawa, Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi ameshuhudia zoezi la utiaji saini mara baada ya kupata taarifa fupi ya mkataba wa ununuzi wa behewa hizo pamoja na maendeleo ya ujenzi wa reli ya kisasa nchini kutoka kwa Mkurugenzi Mkuu wa TRC Ndugu Masanja Kungu Kadogosa kuwa Ujenzi wa reli ya kisasa unaoendelea kwa sasa ni kipande cha Dar es Salaam – Morogoro umefika 95%, Morogoro – Makutupora umefika 81% na Mwanza – Isaka umefika 4%.

Hata hivyo Waziri Mbarawa alisema kuwa katika Behewa hizo 1430 zitakazotengenezwa zipo Behewa 60 za mifugo ambapo Behewa moja itakuwa na uwezo wa kubeba takribani Ngo'mbe 100 ambayo ni sawa na Ngo'mbe 6,000 kwa Behewa 60. Pia zipo behewa 50 maalumu kwa ajili ya kubeba magari ambapo behewa moja itakuwa na uwezo wa kubeba magari madogo 8 ambayo ni sawa na magari 400 kwa behewa 50.

Mhe. Waziri alifafanua kuwa "kutokana na uwezo mkubwa wa reli ya kisasa, behewa hizi zitasaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza mrundikano wa mizigo katika bandari ya Dar es Salaam ambapo treni moja itakuwa na uwezo wa kubeba Tani 10,000 kwa mkupuo ambayo ni sawa na malori 500" alisema Prof. Mbarawa.

Inaendelea Uk. 6

# BEHEWA 1,430 ZA KISASA ZA MIZIGO KUNUNULIWA



Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Mhe. Prof. Makame Mbarawa (wa tano kushoto) akiwa katika picha ya pamoja na uongozi wa TRC wakati wa hafla ya utiaji saini mkataba wa ununuzi wa behewa 1430 za SGR za mizigo katika ukumbi wa mikutano, ofisi ya makao makuu TRC Dar es Salaam Februari 2022.

Inatoka Uk. 5

Katika hatua nyingine, Mhe. Waziri aliwapongeza wafanyakazi wa Shirika la Reli kwa usimamizi mzuri wa mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa na kuwaomba waendelee kuchapa kazi kwa kutumia weledi walionao na jitihada ili kutimiza malengo ya Serikali ya kuhudumia wananchi na kukuza uchumi wa Taifa.

Mkurugenzi Mkuu TRC, Ndugu Masanja Kadogosa katika taarifa yake amesema kuwa,
"Mkataba huu ni wa ununuzi wa Behewa 1430 za mizigo za reli ya kisasa ambao unagharimu Dola za Kimarekani Milioni 127.2, ni mkataba wa miezi 12 yaani mwaka mmoja utakaohusisha usanifu na utengenezaji wa Behewa kwaajili ya kubeba mizigo ya aina mbalimbali kulingana na aina ya behewa na matakwa ya mteja kupitia reli ya kisasa".

Akizungumza katika hafla hiyo, Mkurugenzi mkuu aliweka wazi kuwa aina ya behewa zitakazonunuliwa kupitia mkataba huu ni, Behewa 600 aina CCB (Container Carrier Bogie) kwaajili ya kubeba makasha, Behewa 400 aina ya CLB (Covered Large Bogie) kwaajili ya kubeba mizigo ya jumla ikiwemo Sukari, Saruji, Chumvi, Pamba, Tumbaku na Kahawa, Behewa 190 aina ya PTB (Petroleum Tank Bogie) kwaajili ya kubeba mafuta aina zote, Behewa 70 aina ya HLB (High Large Bogie) kwaajili ya Mabomba, Mbao, Magogo na Vyuma, Behewa 50 aina ya MGB (Motor Goods Bogie) kwaajili ya kubeba magari na Behewa 50 aina ya CWB (Cattle Wagon Bogie) kwaajili ya kubeba Ng'ombe.

Kwa upande wake Mwakilishi wa kampuni ya CRRC ambaye ni Meneja Msaidizi Bw. Tang Yun Pengamesema kuwa "Leo ni siku nzuri kwetu CRRC kwa sababu haikuwa rahisi kufikia hapa, nakumbuka mwaka jana tulishiriki katika mradi wa uboreshaji wa reli ya kati, hivyo tuna ujasiri wa kutosha kusanifu na kutengeneza behewa bora na imara kwaajili yenu" alisema Bw. Peng.

Shirika la Reli Tanzania linatarajia kukamilika kwa manunuzi na kuwasili kwa behewa hayo mapema Februari 2023 ambako kutakwenda sambamba na kukamilika kwa mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa kipande cha pili Morogoro – Makutupora ambacho kwa umbali huo kutaweza kuleta tija na faida katika uendeshaji wa huduma ya usafirishaji mizigo

# KAMATI YA BUNGE YA BAJETI YAIPONGEZA WIZARA NA TRC

Kamati ya Bunge ya Bajeti ikiongozwa na Mwenyekiti wa kamati hiyo Mhe. Daniel Sillo imefanya ziara kukagua mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa – SGR kipande cha Dar es Salaam – Morogoro kuanzia stesheni ya Dar es Salaam hadi Soga mkoani Pwani Machi 7, 2022.

Lengo la ziara hiyo ni kufanya ukaguzi kwaajili ya kujiridhisha na matumizi ya fedha zinazotengwa kutekeleza miradi ya kimkakati ikiwemo ujenzi wa reli ya kisasa. Kamati imefanya ukaguzi huo ikiwa ni hatua mojawapo kuelekea maandalizi ya bajeti ya Serikali kwa mwaka 2022/2023.



Mkurugenzi Mkuu TRC Ndugu Masanja Kadogosa (kulia) akimuelezea Mwenyekiti na wajumbe wa kamati ya bunge ya bajeti kuhusu miundombinu ya treni za mizigo katika stesheni ya reli ya kisasa - SGR Pugu jijini Dar es Salaam Machi 2022.

na hivi leo tumetembelea mradi huu wa SGR kuona fedha zilizotengwa kama zinafanya kazi iliyopangwa na tumeona kazi nzuri imefanyika katika kipande cha Dar es Salaam – Morogoro (km300) imekamilika kwa 95.3%, tunaipongeza serikali ya CCM chini ya Rais Samia Suluhu Hassan lakini pia wizara na TRC tunawapongeza sana" alisema Mhe. Daniel Sillo

Mhe. Sillo amesema kuwa ujenzi wa reli ya kisasa ni muhimu kiuchumi na kijamii, kwa kuwa ujenzi huu unaunganisha Bandari na nchi jirani na kuongeza kuwa kamati hiyo itaendelea kuishauri serikali kutoa fedha kwaajili ya kutekeleza mradi huu mkubwa kwaajili ya maendeleo ya Taifa na mtu mmoja mmoja.

"Lengo la ziara hii ni kutembelea miradi mingi ya kimkakati ambayo serikali imeweka fedha nyingi

Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Mhe. Atupele Mwakibete ameishukuru kamati ya bunge ya bajeti kutembelea mradi wa SGR na imeridhika namna ambavyo serikali imewekeza na kueleza kuwa Serikali imeweka na inaendelea kuweka fedha nyingi katika mradi huo.

"Nimpongeze sana Mhe. Rais Samia kwa kuendelea kutafuta fedha na kuhakikisha mradi wa reli ya kisasa unakamilika, ni zaidi ya Trilioni 7 zimeshalipwa na hakuna mkandarasi anayedai lakini pia ni zaidi ya Trilioni 14.5 ambazo tumeingia mikataba, naamini bunge lilajo litaidhinisha fedha ili watanzania wapate huduma bora" aliongeza Mwakibete

Naye Mkurugenzi wa Shirika la reli Tanzania Masanja Kadogosa ameshukuru ujio wa kamati hiyo kwakuwa Serikali iko katika mpango wa kuandaa bajeti ya mwaka 2022/2023 hivyo ujio wa kamati hiyo umesaidia kwa kiasi kikubwa kuiaminisha kamati hiyo kuhusu kile kinachofanyika

"Tunaishukuru kamati yetu ya bajeti kuja kututembelea, sasa tuko kwenye harakati za kuandaa bajeti, kwahiyo inavyokuja na kujionea kazi inakuwa rahisi sana kuwaelezea kwa sababu wameshaona", alisema Kadogosa

Kadogosa aliongeza kuwa "Ujenzi tulianza na pesa ya ndani lakini baadaye tulipata fedha kutoka taasisi za kifedha na ndio utaratibu tunaoendelea nao, hata kwa kipande tunachoanza nacho sasa Makutupora – Tabora tayari tumeshalipa malipo ya awali Bilioni 600 ambazo zimetoka ni fedha za ndani, na Serikali inaendelea kutafuta fedha kuongeza nguvu"

# KAMATI YA BUNGE YA MIUNDOMBINU YATEMBELEA UJENZI WA SGR MWANZA – ISAKA, WAMPONGEZA RAIS SAMIA

Kamati ya bunge ya kudumu ya miundombinu imetembelea na kukagua maendeleo ya ujenzi wa kipande cha tano cha mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa - SGR Mwanza – Isaka, chenye jumla ya km 341, jijini mwanza. Machi 2022.

Katika ziara hiyo sehemu ya ukaguzi wa miradi mbalimbali ya ujenzi nchini, kamati imetembelea kambi ya mkandarasi iliyopo eneo la Seke wilayani Kishapu mkoani Shinyanga, Kambi ya Fela wilayani Misungwi, Mwanza na kambi ya Malampaka ya Maswa mkoani Simiyu.

Akitoa taarifa ya maendeleo ya mradi mbele ya kamati hiyo meneja mradi wa ujenzi wa SGR Mwanza – Isaka, Mhandisi Machibya Masanja ameeleza kuwa mpaka sasa ujenzi katika kipande hicho umefikia 4.46%.

Aidha, akifafanua juu ya utofauti wa wakandarasi katika vipande tofauti vya utekelezaji wa awamu ya kwanza ya ujenzi wa reli ya kisasa, Mhandisi Machibya amesema kuwa utofauti huo hauwezi kupelekea utofauti wa viwango kwakuwa wakandarasi wote wanajenga kulingana na viwango vilivyoainishwa katika matakwa ya muajiri.

"Tulilizingatia hilo kwasababu, kama tungekuwa na viwango tofauti katika vipande hivi vya mradi, wakati wa kuanza uendeshaji isingewezekana kupitisha treni moja kuanzia Dar es salaam hadi Mwanza, tunachokitaka hata kama reli itajengwa na wakandarasi watatu au wane tofauti, ionekane ni reli moja" alieleza Mhandisi Machibya.

Akieleza juu ya namna ambavyo majaribio ya ubora wa vifaa vya ujenzi yanavyofanyika katika mradi, Mkurugenzi wa Miundombinu ujenzi, Mhandisi Faustine Kataraia ameeleza kuwa zoezi hilo linafanyika kupitia maabara za mshauri Mwelekezi, maabara ya Chuo kikuu cha Dar es salaam na Shirika la Viwango nchini - TBS.

Kwa upande wake Naibu waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Mhe. Atupele Mwakibete amesema kuwa hadi kufikia sasa uwekezaji wa serikali katika ujenzi wa Reli ya kisasa, umefikia Shilingi Trilioni 14.7 na kuwa wakandarasi wanalipwa kwa wakati.



*Kaimu Mkurugenzi wa Miundombinu Ujenzi TRC Mhandisi Machibya Masanja (aliyeshika fimbo) akiwapatia maelezo wajumbe wa kamati ya bunge ya miundombinu kuhusu maendeleo ya madi wa SGR walipofanya ziara Machi 2022.*

"Kuanzia kipande cha kwanza hadi hapa, hakuna mkandarasi anayedai na serikali imeshalipa zaidi ya Shilingi Trilioni 7" alisema Naibu Waziri Mwakibete.

Mara baada ya kuhitimisha ziara hiyo katika kambi ya Mkandarasi ya Malampaka, Maswa mkoani Simiyu, mwenyekiti wa kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, Moshi Selemani Kakoso, amempongeza Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan kwa utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa ambao mpaka sasa awamu ya kwanza inatekelezwa kwa vipande vinne vya ujenzi kati ya vitano.

Hata hivyo, Mhe. Kakoso amewataka wahandisi wazawa waliopewa dhamana ya kusimamia ujenzi wa reli ya kisasa, kuwa wazalendo ili kukamilisha mradi katika viwango vinavyohitajika.

Kwa upande wake mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya TRC, Prof. John Kondoro ameishukuru kamati kwa kutembelea na kukagua ujenzi wa kipande cha tano cha SGR Mwanza – Isaka na kueleza kuwa maelekezo na ushauri wa kamati hiyo ni chachu kwa TRC katika kuendelea kusimamia vyema ujenzi wa mradi huo wa kimkakati.

Utekelezaji wa kipande cha tano cha mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa Mwanza – Isaka ulianza Mei 15, 2021 ambapo mpaka sasa maendeleo ya ujenzi yamefikia 4.46% huku faida mbalimbali zikitajwa kuambatana na utekelezaji wa mradi ikiwemo ajira na maendeleo ya sekta ya viwanda na uwekezaji.

# KAMPENI YA UELEWA KWA JAMII KUHUSU UJENZI WA SGR YAZIDI KUSHIKA KASI MAKUTUPORA – TABORA



*Bw. Leodgard Otaru, Afisa Usimamizi wa masuala ya kijamii, TRC akizungumza na wajumbe wa Serikali ya Kijiji cha Mabondeni, Itigi mkoani Singida, katika kikao cha ndani kabla ya Mkutano wa hadhara na wanakijiji wa Mabondeni Aprili 2022.*

Shirika la Reli Tanzania TRC, limeanza kampeni maalumu ya uelewa kwa jamii kuhusu mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa - SGR, kipande cha tatu cha Makutupora – Tabora, ikihusisha mikoa ya Singida na Tabora ambayo inapitiwa na mradi, Aprili 2022.

Kampeni hiyo iliyoanza mapema mwezi Aprili, mkoani Singida, inahusisha timu ya wataalamu kutoka idara mbalimbali za TRC kwa lengo la kutoa uelewa kwa Viongozi na wananchi katika mikoa hiyo kuhusiana na masuala ya fursa za ajira na biashara, elimu ya awali ya utwaaji ardhi na fidia, ulinzi na usalama, mazingira na masuala mtambuka yatakayoambatana na mradi.

Akizungumza mara baada ya mkutano wa hadhara na wananchi wa mji mdogo wa Manyoni, wilayani Manyoni mkoani Singida, afisa kutoka Kitengo cha Usimamizi wa masuala ya kijamii, Bw. Leodgard Otaru amesema kuwa kwa mkoa wa Singida Kampeni hiyo imefanyika kikamilifu katika Halmashauri ya mji Itigi na halmashauri ya mji Mdogo wa Manyoni na inatarajiwa kufanyika mkoani Tabora kuanzia tarehe 25 Aprili 2022.

"Wananchi wamepokea vizuri kampeni hii na wameonesha ushirikiano mkubwa, kwani katika baadhi ya maeneo wameruhusu mkandarasi aendelee na shughuli za awali za utekelezaji wa mradi kama vile uchukuaji wa sampuli za udongo" aliongeza Bw. Otaru.

Kampeni ya uelewa kuhusu mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa, imekuwa ni moja kati ya hatua muhimu za utekelezaji wa wa mradi huu wa kimkakati ambapo kwa kupitia mikutano ya hadhara wananchi na viongozi wanapata taarifa sahihi za mradi na hatimaye kurahisisha utekelezaji.

Pamoja na wataalamu kutoka TRC, kampeni ya uelewa kuhusu Mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa inajumuisha pia wawakilishi kutoka kampuni ya mkandarasi, akizungumza katika moja ya mikutano ya hadhara wilayani Manyoni, Afisa Uhusiano kutoka Kampuni ya Mkandarasi Yapi Merkezi, Bi. Hamisa Juma ameeleza kuwa pamoja na kutekeleza shughuli za ujenzi katika mradi, mkandarasi pia ana jukumu la kusaidia katika baadhi ya changamoto zinazoikumba jamii inayoishi kando na mradi.

Bi. Hamisa amesema kuwa "utaratibu ni kwamba baada ya kutambua changamoto wanayohitaji mkandarasi asaidie kuitatua, wananchi wawasilishe taarifa katika uongozi wa kijiji ambao utaandika barua kwenda kwa mkandarasi".

Mmoja wa wakazi wa mji Mdogo wa Manyoni, Bi. Sarah Mwampeta ameeleza kuwa wamepokea vizuri ushirikishwaji wa wananchi kupitia kampeni ya uelewa.

"Mradi huu utawapatia ajira vijana katika haya maeneo yetu, lakini pia reli ya kisasa itaturahisishia usafiri ukilinganisha na reli ya zamani ambayo tulikuwa tunasafiri kwa muda mrefu"

Sambamba na zoezi la Kampeni ya uelewa kwa jamii, hatua za awali za ujenzi wa reli ya kisasa Makutupora – Tabora zinaendelea ikiwa ni pamoja na Utambuzi wa maeneo ya ujenzi wa Makambi, ukusanyaji wa mitambo na rasilimali watu pamoja na uchukuaji wa sampuli za udongo katika maeneo ya Kitaraka, Itigi mjini na Kazikazi.

Kampeni hii inafuatia kuanza rasmi kwa shughuli za ujenzi katika kipande cha SGR Makutupora – Tabora ambapo tarehe 12 Aprili 2022, Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa kwa niaba ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan, aliweka jiwe la msingi katika eneo la Cheyo B mkoani Tabora.

# MAFANIKIO YA SHIRIKA LA RELI KATIKA UJENZI WA SGR NDANI YA MWAKA MMOJA WA RAIS SAMIA



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan akiweka jiwe la msingi la mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa - SGR kipande cha Mwanza - Isaka, Fela mkoani Mwanza Juni, 2021.

Umetimu mwaka mmoja tangu Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan aingie madarakani mara baada ya kuapishwa mnamo mwezi machi 2022, ndani ya mwaka mmoja Serikali imeendelea na utekelezaji wa miradi mbalimbali ya kimkakati. Moja kati ya miradi mikubwa inayoendelea kutekelezwa ni ujenzi wa miundombinu ya reli ya kisasa – SGR ambao unatekelezwa katika vipande vinne.

Shirika la Reli Tanzania – TRC ni miongoni mwa mashirika ya Serikali ambayo yameendelea kusimamia maagizo ya Serikali ya awamu ya sita tangu alipoingia madarakani, kwa ushirikiano uliopo kati ya Serikali na Shirika la Reli nchini tumeona mafanikio mengi ambayo Serikali imeacha alama ndani ya siku 365 ya Rais Samia kuwa madarani.

TRC imepewa dhamana ya kutoa huduma ya usafiri wa abiria na usafirishaji wa mizigo kwa njia ya reli, lakini pia imepewa dhamana ya kuendeleza na kusimamia miundombinu ya reli ambapo hivi sasa Shirika linasimamia mradi wa ujenzi wa reli ya Kisasa – SGR awamu ya kwanza Dar es Salaam – Mwanza yenye vipande vitano.

Licha ya Shirika kuwa na jukumu la kusafirisha abiria na mizigo pamoja na kusimamia mradi wa SGR, shirika limekuwa na mafanikio mengi katika uendeshaji wa shirika kiujumla lakini pia katika utekelezaji wa mradi wa SGR. Makala hii itajikita hasa katika upande wa mafanikio katika ujenzi wa reli ya kisasa. Katika upande wa ujenzi wa reli ya kisasa, mafanikio ambayo tumeyashuhudia ni kama ifuatavyo.

## Utekelezaji wa awamu ya kwanza ya ujenzi wa reli ya kisasa – SGR

Rais Samia amefanikiwa kuendeleza awamu ya kwanza ya ujenzi wa SGR kutoka Dar es Salaam hadi Mwanza (km 1,219) ujenzi unatekelezwa katika vipande vitano ambayo ni Dar es Salaam – Morogoro, Morogoro – Makutupora, Makutupora - Tabora na Isaka - Mwanza ambavyo utekelezaji wake unaendelea.

Utekelezaji wa mradi unaenda kwa kasi vipande takribani vinne vikiwa katika hatua za utekelezaji na vipande vingine vikiwa mbioni kukamilika. Kipande cha Dar es Salaam - Morogoro (km 300) ujenzi ukiwa umefikia 96%, Kipande cha Morogoro - Makutupora (km 422) ujenzi ukiwa umefikia 82%, Kipande cha Makutupora - Tabora (km 368) hivi karibuni Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Prof. Makame Mbarawa

**Inaendelea Uk. 11**

# MAFANIKIO YA SHIRIKA LA RELI KATIKA UJENZI WA SGR NDANI YA MWAKA MMOJA WA RAIS SAMIA




Inatoka Uk 10

aliweka jiwe la msingi la ujenzi kwa niaba ya Rais Samia Suluhu Hassan na hivi karibuni ujenzi unatarajiwa kuanza ambapo utagharimu kiasi cha Shilingi za kitanzania Trilioni 4.406. Kipande cha Tabora - Isaka (km 165) kipande hiki kipo katika hatua za manunuzi, kipande cha Isaka - Mwanza (km 341) ujenzi ukiwa umefikia 4.46%. Hadi kufikia sasa uwekezaji wa Serikali katika ujenzi wa reli ya kisasa umefikia Shilingi Trilioni 14.7.

Mapema mwezi Februari 2022, TRC ilisainina mkataba na kampuni ya CRRC International kutoka Nchini China kwaajili ya ununuzi wa Behewa 1430 za mizigo zitakazotumika katika reli ya kisasa ambapo mkataba unagharimu Dola za Kimarekani Milioni 127.2, mkataba utakaotekelezwa kwa muda wa miezi 12 yaani mwaka mmoja.

Shirika linatarajia kuwa na Behewa 600 aina CCB (Container Carrier Bogie) kwaajili ya kubeba makasha, Behewa 400 aina ya CLB (Covered Large Bogie) kwaajili ya kubeba mizigo ya jumla ikiwemo Sukari, Saruji, Chumvi, Pamba, Tumbaku na Kahawa, Behewa 190 aina ya PTB (Petroleum Tank Bogie) kwaajili ya kubeba mafuta aina zote, Behewa 70 aina ya HLB (High Large Bogie) kwaajili ya Mabomba, Mbao, Magogo na Vyuma, Behewa 50 aina ya MGB (Motor Goods Bogie) kwaajili ya kubeba magari na Behewa 50 aina ya CWB (Cattle Wagon Bogie) kwaajili ya kubeba Ng'ombe.

Hata hivyo, Shirika limesaini Mkataba na Kampuni ya EUROWAGON ya Uturuki tarehe 1 Oktoba, 2020 kwa ajili ya ununuzi wa vichwa viwili (2) vya treni ya umeme na behewa 30 za abiria. Mkataba huu una thamani ya EURO Milioni 26.60. Mkandarasi anatarajiwa kuleta vifaa hivyo mwezi Aprili, 2022.

Pia, kuna mkataba kati ya TRC na kampuni ya Hyundai Rotem ya Korea kusini kwaajili ya ununuzi wa vichwa vya treni vya umeme 17 na seti za treni za kisasa (Electric Multiple Unit-EMU) 10 na 'Locomotive simulator' 1 ya umeme umesainiwa tarehe 14 Julai, 2021 kwa gharama ya Dola za Marekani milioni 295.74. Kazi hii yote inatarajiwa kuchukua miezi 34.

Halikadhalika, Shirika limesaini Mkataba na Kampuni ya SSRST ya Korea kusini kwaajili ya ununuzi wa behewa 59 ya abiria tarehe 23 Septemba, 2020. Malipo ya awali yameshafanyika na hadi January, 2022 kazi ya matengenezo imefikia asilimia 60. Mkataba huu ni wa miaka miwili utakamilika tarehe 22 Septemba, 2022.

Kwa sasa Shirika la Reli imekamilisha kuunganisha reli ya kisasa - SGR njia kuu kipande cha Dar es Salaam - Morogoro, na majaribio ya mifumo mbalimbli yananendelea ikiwemo mifumo ya umeme.

Shirika la Reli Tanzania linaendelea na juhudi ya kufanya kampeni mbalimbali kwa wananchi za usalama wa njia za reli pamoja na kutoa elimu juu ya uelewa wa kuilinda miundombinu ya reli ili kuepusha madhara yatikanayo na watu kupata ajali ama njia kuharibika na kusababisha matokeo hasi ya usafirishaji.

yapı merkezi
LATRA
Tanzania Commercial Bank
Growing stronger together
GBP
SMH RAIL
. . . extending life
NBC
Benki ya Taifa ya Biashara
Daima Karibu Nawe.
NMB
Karibu yako
CRDB BANK
Tunakusikiliza
tigo pesa
NSSF
We Build Your Future
PUMA ENERGY
AKO
AKO GROUP LIMITED
AFRICA'S NO.1 CHOICE
azam
Wheat Flour
BRAVO
LOGISTICS
Kamal Steel
Posta
Let's Go!
TPA
TANZANIA PORTS AUTHORITY
NIC
SISI NDIYO BIMA

**SHIRIKA LA RELI TANZANIA**
**Barabara ya Sokoine**
**S.L.P 76959**
**Dar es Salaam**
**TANZANIA**
**Barua pepe; info@trc.co.tz**
**Simu ya Bure; 0800 110 042**

**Limeandaliwa na Kitengo cha Uhusiano**
**SHIRIKA LA RELI TANZANIA**

| | |
|---|---|
| **MHARIRI MKUU** | **Jamila Mbarouk** |
| **MHARIRI MSAIDIZI** | **Sami Omary** |
| **MAKALA** | **Aziza Charles & Hemed Mohamed** |
| **HABARI** | **Amina Juma Mariam Katunge** |
| **PICHA** | **Seleman Kadiko Hassan Said** |

**tzrailways TRC Reli TV www.trc.co.tz**

**Reli Yetu | Maendeleo Yetu | Taifa Letu #TRCMpya**